JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA SAME

Simu: +255784512 774
+255767512774
+255764399385

Email: ntengasecondary1996@gmail.com

Shule ya Sekondari Ntenga,
S.L.P 263,
Same.
KILIMANJARO

Tarehe……/……./20….

FOMU NA ……..…

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NTENGA KWA MWAKA WA MASOMO 2020.

Ndg, ……..

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari **Ntenga** kwa mwaka 2021. Shule hii ipo umbali wa kilometa hamsini (50) mashariki mwa mji wa **Same** katika mkoa wa **Kilimanjaro**. Shule hii inachukua wanafunzi wa jinsia zote (**me na ke**). Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 04/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 11/01/2021 .

Nakupongeza kwa dhati pia ninakukukaribisha sana katika shule hii. Utapata likizo mara mbili kwa mwaka na utalazimika kuwa zamu ya kulinda shule ukiwa kidato cha kwanza **mara moja** katika muda wote wa miaka minne.

1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.1 SARE YA SHULE.

Sare ya shule kwa mwaka wa masomo 2021 itakuwa kama ifuatavyo;

A. WAVULANA

- ✓ Suruali rangi ya **Kaki** Jozi mbili
- ✓ Shati Jeupe mikono mifupi jozi mbili.
- ✓ Tai rangi ya **Kaki** jozi mbili **zenye nembo ya shule**
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi, vya kufunga kwa kamba/Gidamu Jozi mbili.
- ✓ Tisheti rangi **Nyeusi** yenye nembo ya shule.
- ✓ Soksi nyeusi jozi mbili.
- ✓ Sweta rangi **Nyeusi** lenye nembo ya shule

B. WASICHANA

- ✓ Sketi rangi **ya Kaki**
- ✓ Mshono wa siketi ni Linda Boksi, iwe yenye urefu wa kuvuka magoti kiasi cha sentimita 10
- ✓ Tai rangi ya **Kak**i jozi mbili zenye nembo ya shule
- ✓ Shati jeupe mikono mifupi jozi mbili.
- ✓ Viatu vyeusi, vya ngozi vyenye kisigino kifupi , vya kufunga kwa kamba/gidamu jozi mbili.
- ✓ Tisheti rangi **Nyeusi** yenye nembo ya shule.
- ✓ Sweta rangi **Nyeusi** lenye nembo ya shule.
- ✓ Soksi nyeupe jozi mbili.

(***Kwa watakaovaa Hijabu na nusu kanzu ziwe ndefu za kuridhisha rangi nyeupe yenye nembo ya shule. Na sketi ziwe ndefu hadi kwenye visigino vya miguu rangi ya kaki***

C. TRACK SUIT

Kila mwanafunzi anapaswa kuvaa track suit ya rangi ya **Bluu** siku ya Ijumaa wakati wa michezo tu. Pia raba nyeupe isiyo na nakshi yoyote na ya kufunga na kamba/gidamu.

NB: ***Ni Muhimu kila mwanafunzi kuwa na jozi mbili kwa kila sare inayohitajika shuleni ili kuepusha utoro unaotokana na kadhia ya kuwa na sare jozi moja. Kumekuwepo na usumbufu wa mara kwa kwa unaotokana na ufinyu wa kuwa na sare jozi moja. Aidha ni vyema mzazi azingatie ubora wa kitambaa cha mtoto, vitambaa visivyo bora vinachakaa na kufubaa muda mfupi sana kiasi kwamba kinakuwa na rangi tofauti kabisa.***

Sampo ya kitambaa ni kama kinavyoonekana kwenye picha hapo chini

D. VIFAA VYA DARASANI

- ✓ Daftari kumi (10) Counter Book ukubwa wa 3Quires
- ✓ Kalamu za bluu au nyeusi nyingi za kutosha
- ✓ Mkebe wa mahesabu (mathematical set) mmoja
- ✓ Penseli na rula.

2.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu **Na 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na. 10** ya mwaka **1995.** Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya **Rais -TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongzi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na Jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
e) Kutunza usafi wa mazingira ya shule, mavazi, na usafi wa mwili kwa ujumla.
f) Kuvaa sare ya shule muda wote wa siku za masomo na pale unapotakiwa kufanya hivyo.
g) Kuzingatia ratiba ya shule muda wote.
h) Kutunza mali za umma kikamilifu.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababishakusimamishwa au kufukuzwa shule.

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
e) Kupiga au kupigana.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma. Mf meza, kiti, n.k
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au Kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani au usalama wa shule.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

n) Kutumia lugha chafu na yenye matusi ambayo inasababisha shambulio la aibu.

3.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

…….

OSCAR A. MASHELLE
MKUU WA SHULE